



**NATIONWIDE
CHILDREN'S**

When your child needs a hospital, everything matters.™

AKAUNTI ZA WAGONJWA – KULIPA BILI YA HOSPITALI Sera na Taratibu (SWAHILI)

Kichwa cha Sera: MSAADA WA KIFEDHA	Tarehe ya Kuanza Kutumika 01/01/2016
Kifungu: Huduma za Kifedha za Wagonjwa	Tarehe ya Marekebisho: 17/4/2017, 4/12/2017, 7/3/2019, 15/10/2019, 19/11/2019, 1/1/2021

MADHUMUNI NA UPEO:

Madhumuni ya sera hii ni kuweka taratibu za kawaida za kubainisha msaada wa kifedha kwa wagonjwa wa Nationwide Children's Hospital (Hospitali ya Kitaifa ya Watoto) (Nationwide Children's) na Huluki ambazo ni Washirika wake zinazohitaji msaada wa kifedha. Sera hii inaweka mchakato wa wafanyakazi wa Idara ya Patient Accounts, wafanyakazi wengine wa hospitali na wawakilishi wa Muuzaji wa Nje kubainisha wagonjwa na familia zilizotimiza masharti ya matibabu ya bure au yaliyopunguzwa bei. Idara ya Patient Accounts ya Nationwide Children's Hospital ina mamlaka ya mwisho ya kubainisha iwapo mtu anatimiza masharti ya msaada wa kifedha na kubainisha kuwa hatua adilifu zimechukuliwa kabla Nationwide Children's hiyo kushiriki katika Vitendo vya Ajabu vya Kukusanya. Masharti ya msaada wa kifedha yanatumika kwa wagonjwa wote bila kujali mbari, rangi, imani, kabila, asili ya kitaifa, umri, jinsia, mwelekeo wa kingono, utambulisho wa jinsia, dini au ulemavu.

Huduma zinazoshughulikiwa na sera hii ni pamoja na dharura zote na Huduma zingine za Lazima za Matibabu zinazotolewa na Nationwide Children's Hospital na Huluki ambazo ni Washirika wake.

Nationwide Children's Hospital itatoa, bila kubagua, huduma za kukabiliana na hali za matibabu ya dharura kwa watu bila kujali iwapo wametimiza masharti ya kupokea msaada wa kifedha. Nationwide Children's Hospital itatii Sheria ya Matibabu ya Dharura na Kazi (EMTALA) kwa kutoa uchunguzi wa matibabu na matibabu ya utulivu na kurejeza na kuhamisha mgonjwa kwa hospitali nyingine, inapofaa na kutoa huduma za dharura kulingana na 42 CFR 482.55 (au kanuni nyingine inayochukua nafasi yake). Nationwide Children's Hospital hairuhusu vitendo vyovyote ambavyo vinaweza kumvunja moyo mtu asitafute huduma za dharura za matibabu, kama vile kuhitaji kwamba wagonjwa wa idara ya dharura walipe kabla ya kupokea matibabu ya hali za matibabu ya dharura au kwa kukubali shughuli za ukusanyaji wa deni ambazo zinaweza kutatiza utoajiwa huduma za matibabu ya dharura, bila kubagua.

UFAPANUZI:

Huluki Zinazoshirikishwa – Kampuni zinazoshirikishwa zinazomilikiwa na Nationwide Children's Hospital zinazotoa huduma za dharura na Huduma zingine za Lazima za Matibabu kwenye hospitali ikiwa ni pamoja na Washirika wa Unusukaputi ya Watoto, Taasisi ya Rediolojia ya Watoto, Washirika wa Upasuaji wa Watoto, Chama cha Taaluma ya Watoto na Washirika wa Patholojia ya Watoto wa Columbus. Ingawa huluki ya Utendaji wa Jamii ya Watoto hautoi huduma kwa mgonjwa kwenye hospitali, inamilikiwa na Nationwide Children's Hospital na inatoa msaada wa kifedha kulingana na sera hii.

Kiasi Kinachotozwa kwa Kawaida (AGB) – Kiasi kinachotozwa kwa kawaida na Nationwide Children's kwa wagonjwa walio na bima.

Wauzaji wa Nje – Makampuni yaliyoajiriwa kama mawakala kuhusu malipo na ukusanyaji.

Vitendo vya Ajabu vya Kukusanya – Hatua zinazochukuliwa na Nationwide Children's dhidi ya mtu zinazohusiana na kutoza malipo ya bili ya huduma zilizo katika Sera hii ya Msaada wa Kifedha zilizobainishwa katika 26 CFR 1.501(r)-6(b) (au kanuni nyingine inayochukua nafasi yake).

Ukubwa wa Familia – Utajumuisha mgonjwa, mwanandoa wa mgonjwa, bila kujali iwapo mwanandoa anaishi nyumbani na watoto wote wa mgonjwa, halisi au wa kuasili, chini wa umri wa miaka kumi na minane wanaoishi nyumbani. Iwapo mgonjwa hajafikisha umri wa miaka kumi na minane, "familia" itajumuisha mgonjwa, mzazi/wazazi halisi au wa kuasili wa mgonjwa (bila kujali iwapo wanaishi nyumbani) na watoto wa wazazi, halisi au wa kuasili walio chini ya umri wa miaka kumi na minane wanaoishi nyumbani.

FAP – Sera ya Msaada wa Kifedha.

Kiwango cha Umaskini cha Shirikisho (FPL) – Kipimo kilichobainishwa na serikali ya Marekani kulingana na mapato ya mwaka na ukubwa wa familia ili kuonyesha upeo wa umaskini.

Jumla ya Malipo – Kiasi kinachotazwa kwa ajili ya huduma za afya.

Jumla ya Mapato – Jumla ya mapato kabla ya makato.

Huduma ya Lazima ya Kimatibabu – Huduma za matibabu au bidhaa zinazohitajika kuzuia, kutambua au kutibu ugonjwa, jeraha, hali, maradhi au dalil zake na ambazo zinatimiza viwango vinavyokubaliwa vya dawa.

Wajibu wa Mgonjwa – Kiasi ambacho mtu anawajibika baada ya malipo yote ya bima (ikiwa ni pampja na walipaji wa biashara na serikali), makato na mapunguzo kuwekwa kwa bili ya mgonjwa.

MAAGIZO:

Masharti ya Kujiunga

Mgonjwa yeyote anayetafuta kupokea matibabu ya dharura au Huduma zingine za Lazima za Matibabu katika Nationwide Children's anaweza kutuma ombi la kupokea msaada wa kifedha; hata hivyo, mbinu inayotumika kutathmini uwezo wa kutimiza masharti inaweza kutofautiana kulingana na mahali anakotoka mgonjwa iwapo anatafuta huduma isiyo ya dharura.

Wakaazi wa Ohio wanaoomba msaada wa kifedha lazima watume ombi la usaidizi wa serikali kwanza unaopatikana pamoja na, lakini si Ohio Medicaid tu (Mpango wa Healthy Start and Healthy Families), Mpango wa Uhakikisho wa Huduma ya Hospitali ya Ohio (HCAP) na msaada wa Bodi ya matumizi ya na Pombe, Dawa za Kulevya na Afya ya Akili (ADAMH). Wakaazi wa Ohio wasio tozwa ushuru wa Usalama wa Jamii na Huduma ya Medicare lazima wawasilishe fomu ya 4029 iliyojazwa, "Ombi la Kutotozwa Ushuru wa Usalama wa Jamii na Huduma ya Medicare na Ondoleo la Manufaa" ili kuondoa masharti haya. Wagonjwa ambao ni wakazi wa Ohio na hawajitimiza masharti ya kupokea manufaa chini ya mipango hii na wagonjwa ambao si wakazi wa Ohio ambao wanapokea huduma za matibabu ya dharura katika Nationwide Children's huenda wakatimiza masharti ya kupokea msaada wa kifedha kulingana na Jumla ya Mapato na Ukubwa wa Familia kama ifuatavyo:

- Mapato ya 200% au ya chini ya Kiwango cha Umaskini Kilichobainishwa na Shirikisho (FPL) yataondolewa katika 100% ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa.
- Mapato ya kati ya 201% na 250% ya FPL yataondolewa katika 80% ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa.
- Mapato ya kati ya 251% na 300% ya FPL yataondolewa katika 60% ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa.
- Mapato ya kati ya 301% na 400% ya FPL yataondolewa katika 45% ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa.

Wakazi wa Ohio wenye mapato ya familia yanayozidi 200% ya FPL lakini chini ya 450% ya FPL ambao bili yao kwenye Nationwide Children's inazidi 20% ya mapato ya kila mwaka ya familia watachukuliwa kuwa hawana uwezo wa kulipa gharama zao za matibabu kwa madhumuni ya sera hii. Familia ambazo hazina uwezo wa kulipa gharama zao za matibabu zitastahiki kupata punguzo la juu kwenye malipo ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa la kiasi ambacho kitafanya malipo ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa ya bili zote za Nationwide Children's yawe sawa na asilimia (%) ya mapato ya kila mwaka ya familia kama ilivyobainishwa hapa chini:

- Mapato ya 200% au ya chini ya Kiwango cha Umaskini Kilichobainishwa na Shirikisho (FPL) yataondolewa katika 100% ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa.
- Mapato ya kati ya 201% na 250% ya FPL yataondolewa hadi kuwa salio sawa na 5% ya mapato ya kila mwaka ya familia.
- Mapato ya kati ya 251% na 300% ya FPL yataondolewa hadi kuwa salio sawa na 7% ya mapato ya kila mwaka ya familia.

- Mapato ya kati ya 301% na 450% ya FPL yataondolewa hadi kuwa salio sawa na 10% ya mapato ya kila mwaka ya familia.

Watu ambao si wakaazi wa Ohio Marekani wanaomba msaada wa kifedha kwa huduma ya matibabu isiyo ya dharura lazima awe ameidhinishwa mapema kupokea msaada wa kifedha kabla ya kupokea huduma hiyo isiyo ya dharura. Mchakato wa kuidhinishwa mapema utahitaji mtu kuwasilisha sababu za kimatibabu kuhusu ni kwa nini huduma zitolewe katika Nationwide Children's kuliko katika kituo cha afya cha jimbo ambako mgonjwa anatoka. Sababu hizi zitakaguliwa na Nationwide Children's na wagonjwa waliobainishwa na hispitali hii wawe wamewasilisha sababu zinazofaa za kitiba huenda wakatimiza masharti ya msaada wa kifedha kulingana na Jumla ya Mapato na Ukubwa wa Familia kama ifuatavyo:

- Mapato ya 200% au ya chini ya Kiwango cha Umaskini Kilichobainishwa na Shirikisho (FPL) yataondolewa katika 100% ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa.
- Mapato ya kati ya 201% na 250% ya FPL yataondolewa katika 80% ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa.
- Mapato ya kati ya 251% na 300% ya FPL yataondolewa katika 60% ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa.
- Mapato ya kati ya 301% na 400% ya FPL yataondolewa katika 45% ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa.

Wakazi wasio wa Marekani wanaomba msaada wa kifedha kwa huduma isiyo ya dharura lazima waidhinishwe mapema kwa msaada wa kifedha kabla ya kupokea huduma hiyo isiyo ya dharura kwa mujibu wa Sera za Nationwide Children's na Taratibu za Wagonjwa wa Kimataifa wa Kupokea Msaada. Kamati ya Uongozi ya Nationwide Children's ya Wagonjwa wa Kimataifa hubainisha masharti ya kimataifa ya mgonjwa kwa huduma za hisani kulingana na vigezo kadhaa, ikiwa ni pamoja na huduma ya matibabu inayohitajika, uwezekano wa huduma hiyo kufaulu kutatua hali za ugonjwa uliopo na kusimamiwa vizuri baada ya matibabu hayo, iwe Nationwide Children's ina uwezo wa kipekee wa kutibu, upatikanaji wa huduma hizi katika nchi ya makaazi ya mgonjwa, vikwazo vya bajeti na vigezo vingine kama hivyo ambavyo Kamati ya Uongozi inaweza kubainisha kuwa yanafaa kuhakikisha nyenzo za huduma za hisani za Nationwide Children's za visa vya kimataifa zinatumia kwa ufanisi na usahihi zaidi. Maelezo kuhusu upatikanaji wa huduma ya hisani kwa wagonjwa wa kimataifa yanapatikana kwa kuwasiliana na Sehemu ya Mapokezi ya Nationwide Children's.

Wapokeaji wa Medicaid wanaopokea Huduma ya Lazima ya Kimatibabu ambayo haishughulikiwi na Medicaid itakuwa na 100% ya Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa kwa Huduma hii ya Lazima ya Kimatibabu kiotomatiki inapoondolewa. Ombi la msaada wa kifedha halitahitajika katika hali hizi.

Familia zitakazotoa fomu iliyojazwa ya 4029 ya IRS au hati zingine kwa Idara ya Akaunti za Wagonjwa ya Nationwide Children's zinazotimiza masharti ya Nationwide Children's ambazo zinathibitisha kuwa familia imeondoa haki yake ya kupokea manufaa ya serikali kwa sababu ya uhusiano wa kidini wa familia, zitastahiki kupata punguzo la Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa linalolingana na lile linalotolewa chini ya mpango huu wa FAP kwa wale wanaopata mapato kati ya 301% na 400% ya FPL. Ombi la msaada wa kifedha halitahitajika katika hali hizi.

Familia zenye anwani ya "Wasio na Makao" zitastahiki kupata punguzo la 100% la Sehemu ya Malipo Yanayostahili Kulipwa na Mgonjwa. Ombi la msaada wa kifedha halitahitajika katika hali hizi.

Idara ya Akaunti za Wagonjwa ya Nationwide Children's itakuwa na mamlaka ya mwisho ya kubaini hali ya kutimiza masharti ya kupokea msaada wa kifedha chini ya sera hii.

Msingi wa Kutathmini Kiasi cha Pesa Zinazotozwa Wagonjwa

Kiasi cha pesa zinazotozwa wagonjwa wanaostahiki kupata msaada wa kifedha chini ya mpango huu wa FAP kwa ajili ya huduma za dharura na Huduma za Kimatibabu Zinazohitajika hakitazidi kiasi cha AGB. Nationwide Children's hutathmini AGB kwa kutumia mbinu ya "Look-Back", jinsi inavyobainishwa katika sheria za nchi, kulingana na madeni yote yanayoruhusiwa na ada za huduma za Medicare na watoa huduma wote wa bima za afya wa kibinafsi katika kipindi cha miezi 12, ikigawanywa na Gharama za Jumla za Nationwide Children's za madeni hayo. Nationwide Children's husasisha tathmini zake za AGB mnamo tarehe 1 Januari ya kila mwaka kwa kutumia data ya kipindi cha miezi 12 kinachokamilika tarehe 30 Septemba kilichotangulia kabla ya tarehe hiyo ya Januari 1. Mwaka wa 2021, AGB ni sawa na 80.1%

Mtu anayetimiza masharti ya kupata msaada wa kifedha hutozwa tu kiasi cha pesa ambacho anastahili kulipa mwenyewe, baada ya mapunguzo na makato yote (ikiwa ni pamoja na mapunguzo yanayopatikana chini ya mpango wa FAP) kutumika na kuondolewa kwa kiasi chochote cha pesa kilichofidiwa na watoa huduma za bima (ikiwa ni pamoja na walipaji wa kibiashara na wa serikali).

Mbinu ya Kutuma Ombi la Msaada wa Kifedha

Ili kuzingatiwa katika mchakato wa kupokea msaada wa kifedha, ni lazima mtu atume ombi la msaada wa kifedha kwa Idara ya Akaunti za Wagonjwa ya Nationwide Children's. Watu wanaotafuta msaada wa kifedha chini ya sera hii katika kiwango cha punguzo la -100% (yaani, watu ambao mapato ya familia yao ni 200% au chini ya FPL) lazima wajaze fomu ya Ombi la Msaada wa Kifedha na watoe maelezo na hati zilizoorodheshwa kwenye fomu ya Ombi la Msaada wa Kifedha. Watu wengine wote wanaotuma maombi wanaweza kutoa maelezo yanayohitajika kwa Idara ya Patient Accounts kupitia kwa simu, ombi la kuandika kwa karatasi halitahitajika. Nationwide Children's inahifadhi haki ya kuomba nakala ya stakabadhi za malipo, W-2 na hati za kulipa ushuru.

Ombi la Msaada wa Kifedha (iwe kwa maandishi au kupitia kwa simu, jinsi inavyobainishwa hapo juu) lazima liwe kama ifuatavyo:

- Huduma za wagonjwa wanaotibiwa na kuruhusiwa kwenda nyumbani kwa wagonjwa walio katika kiwango cha 100% au cha chini ya FPL hulipwa na HCAP na kwa hivyo, zinahitaji kuombwa upya baada ya kila siku 90 kuanzia tarehe ya kwanza ya kupokea huduma. Huduma za hospitalini za wagonjwa wanaotibiwa na kuruhusiwa kwenda nyumbani zinahitaji kuombwa upya kila baada ya siku 180 kuanzia kwa tarehe ya kwanza ya kupokea huduma. Watu wanaopokea manufaa ya mpango wa Msaada wa Ulemavu (DA) au mpango uliochukua nafasi yake chini ya HCAP lazima watume ombi jipya kila mwezi.
- Kila tukio la mgonjwa kulazwa hospitalini, isipokuwa iwapo mgonjwa amelazwa ndani ya siku 45 za kuruhusiwa kwenda nyumbani kwa ajili ya matibabu ya ugonjwa ule, lazima liwe kwenye ombi lake tofauti la msaada wa kifedha. Matukio ya baadaye ya kulazwa tena hospitalini yanaweza kuwa kwenye ombi sawa, lakini iwapo tu yanatokea ndani ya siku 45 na kwa ajili ya matibabu ya ugonjwa unachusiana. Akaunti za wagonjwa wanaotibiwa na kuruhusiwa kwenda nyumbani zinaweza kuongezwa kwenye ombi ambalo lina akaunti ya mgonjwa anayelazwa hospitalini, lakini ziara za kumtembelea mgonjwa aliyelazwa hospitalini haziwezi kuongezwa kwenye ombi ambalo akaunti za wagonjwa wanaotibiwa na kuruhusiwa kwenda nyumbani.

Nationwide Children's haitumii hali za awali za kutimiza masharti ya mpango wa FAP ili kubaini iwapo mtu anatimiza masharti ya kupata msaada wa kifedha chini ya sera hii.

Hali ya Kudhaniwa ya Kutimiza Masharti ya Kupokea Msaada wa Kifedha

Nationwide Children's Hospital inaweza kutumia mtu mwingine kufanya ukaguzi wa maelezo ya mgonjwa ili kutathmini hali ya kutimiza masharti ya FAP kwa msaada wa kikarimu zaidi unapopatikana chini ya mpango wa FAP. Uchanganuzi na ukaguzi huu hutumia muundo wa ubashiri unaotambulika na sekta ya huduma ya afya. Ukaguzi kama huo hautatumiwa kubaini hali za kukisiwa za kutimiza masharti ya kupokea msaada wa ukarimu zaidi unapatikana chini ya FAP.

Hatua Zinazoweza Kuchukuliwa Iwapo Deni Halitalipwa

Nationwide Children's itafanya kila juhudi ili kukusanya deni na kufanya kila jitihada zinazowezezekana ili kubaini iwapo mtu anatimiza masharti ya mpango wa FAP kabla ya kuanza kutumia Hatua Zisizo za Kawaida za Ukusanyaji wa Madeni. Jitihada kama hizo zinazowezezekana zitajumuisha kutuma taarifa na kupiga simu kwa mtu anayehusika katika ratiba iliyobainishwa hapa ndani ya siku 120 baada ya mgonjwa kuruhusiwa kwenda nyumbani. Nationwide Children's inaweza kutumia huduma za Mtoa Huduma wa Nje ili kusaidia katika ukusanyaji wa deni.

Siku 0 hadi 30	Taarifa ya kwanza ya malipo hutumwa, pamoja na ilani iliyoandikwa ya kuarifu kuwa msaada wa kifedha unapatikana, fomu ya ombi la FAP na jinsi ambavyo mtu anaweza kupata msaada wa mchakato wa kutuma ombi la FAP.
Siku 31 hadi 60	Taarifa ya pili ya malipo hutumwa, pamoja na muhtasari wa lugha rahisi wa FAP na ilani ya kuarifu kuwa Nationwide Children's inanuia kuripoti akaunti ambayo haijalipwa kwa ofisi ya ukusanyaji wa madeni iwapo kiasi kama hicho cha pesa hakitalipwa ndani ya siku 365

	kuanzia tarehe ya kupokea taarifa ya malipo baada ya mgonjwa kuruhusiwa kwenda nyumbani. Zaidi ya hayo, simu moja itapigwa ili kumwarifu mtu moja kwa moja kuhusu mpango wa FAP wa Nationwide Children's na jinsi ambavyo mtu anaweza kupata usaidizi wa mchakato wa kutuma ombi la FAP.
Siku 61 hadi 90	Taarifa ya tatu ya malipo hutumwa, pamoja na muhtasari wa lugha rahisi wa FAP na ilani ya kuarifu kuwa Nationwide Children's inanuia kuripoti akaunti ambayo haijalipwa kwa ofisi ya ukusanyaji wa madeni iwapo kiasi kama hicho cha pesa hakitalipwa ndani ya siku 365 kuanzia tarehe ya kupokea taarifa ya kwanza ya malipo baada ya mgonjwa kuruhusiwa kwenda nyumbani. Zaidi ya hayo, simu moja itapigwa ili kumwarifu mtu moja kwa moja kuhusu mpango wa FAP wa Nationwide Children's na jinsi ambavyo mtu anaweza kupata usaidizi wa mchakato wa kutuma ombi la FAP.
Siku 91 hadi 120	Taarifa ya nne ya malipo hutumwa, pamoja na muhtasari wa lugha rahisi wa FAP na ilani ya kuarifu kuwa Nationwide Children's inanuia kuripoti akaunti ambayo haijalipwa kwa ofisi ya ukusanyaji wa madeni iwapo kiasi kama hicho cha pesa hakitalipwa ndani ya siku 365 kuanzia tarehe ya kupokea taarifa ya kwanza ya malipo baada ya mgonjwa kuruhusiwa kwenda nyumbani. Zaidi ya hayo, simu mbili zitapigwa ili kumwarifu mtu moja kwa moja kuhusu mpango wa FAP wa Nationwide Children's na jinsi ambavyo mtu anaweza kupata msaada wa mchakato wa kutuma ombi la FAP.

Zaidi ya ilani iliyoandikwa kwa maandishi ya kuarifu kuwa msaada unapatikana, fomu ya kutuma ombi la FAP na maelezo kuhusu jinsi ambavyo mtu anaweza kupata usaidizi wa mchakato wa kutuma ombi la FAP, taarifa zote za malipo zitajumuisha anwani ya tovuti ya moja kwa moja ambapo nakala za FAP, fomu ya kutuma ombi la FAP na muhtasari wa lugha rahisi wa mpango wa FAP zinaweza kupatikana.

Nationwide Children's inaweza kuripoti akaunti ambazo hazijalipwa kwa ofisi ya ukusanyaji wa madeni baada ya mwaka mmoja (1) kuanzia tarehe ya kupokea taarifa ya kwanza ya malipo baada ya mgonjwa kuruhusiwa kwenda nyumbani. Iwapo bili za mtu zitajumuishwa ili kushughulikia matukio mengi ya matibabu, akaunti ambayo haijalipwa haitaripotiwa kwa ofisi ya ukusanyaji wa madeni hadi angalau baada ya siku 120 baada ya kupokea taarifa ya kwanza ya malipo baada ya mgonjwa kuruhusiwa kwenda nyumbani kwa ajili ya tukio jipya la matibabu lililojumuishwa kwenye bili ya jumla.

Iwapo mtu atatumia ombi la FAP ambalo halijakamilika wakati wa kipindi cha kutuma ombi (yaani, siku 240 baada ya kupokea taarifa ya kwanza ya malipo baada ya mgonjwa kuruhusiwa kwenda nyumbani), Nationwide Children's itampa mtu ilani iliyoandikwa kwa maandishi ambayo yanabainisha maelezo ya ziada na/au hati zinazohitajika chini ya mpango wa FAP au fomu ya kutuma ombi la FAP ambayo ni lazima yawasilishwe ili kukamilisha ombi la mpango wa FAP pamoja na anwani ya mawasiliano ya idara ya Nationwide Children's ambayo inaweza kutoa maelezo kuhusu mpango wa FAP na ambayo inaweza kutoa usaidizi wa mchakato wa kutuma ombi. Nationwide Children's itasimamisha Hatua yoyote Isiyo ya Kawaida ya Ukusanyaji wa Madeni (na panapowezekana, kuwafahamisha Watoa Huduma wake wa Nje kusimamisha juhudi kama hizo) hadi Nationwide Children's itakapobainisha iwapo mtu anatumia masharti ya kupokea msaada wa kifedha chini ya mpango wa FAP au mtu atakapokosa kujibu maombi ya kutoa maelezo ya ziada na/au hati ndani ya kipindi cha muda unaofaa.

Baada ya kupokea ombi lililokamilishwa la FAP wakati wa kipindi cha kutuma ombi, Nationwide Children's itabainisha iwapo mtu anatumia masharti ya mpango wa FAP kwa ajili ya huduma na kumwarifu mtu kupitia kwa maandishi kuhusu ubainishaji huu wa hali ya kutimiza masharti (ikiwa ni pamoja na, panapowezekana, msaada ambao mtu anatumia masharti ya kupata) na msingi wa ubainishaji huu. Iwapo mtu atabainishwa kuwa anatumia masharti ya kupokea msaada mwingine kando na huduma isiyolipishwa, Nationwide Children's:

- Itampa mtu taarifa ya malipo ambayo inaonyesha kiasi cha pesa ambacho anadaiwa kwa ajili ya huduma kama mtu anayetimiza masharti ya FAP na jinsi kiasi hicho cha pesa kilivyobainishwa. Taarifa kama hiyo ya malipo itaelezea pia jinsi ambavyo mtu anaweza kupata maelezo kuhusiana na AGB kwa ajili ya huduma.
- Kumrejeshea mtu kiasi chochote cha pesa ambacho amelipa kwa ajili ya huduma kinachozidi kiasi cha pesa anachostahili kulipa mwenyewe kama mtu anayetimiza masharti ya FAP.
- Kuchukua hatua zote zinazofaa ambazo zinapatikana ili kubatilisha Hatua zozote Zisizo za Kawaida za Ukusanyaji wa Madeni zilizochukuliwa dhidi ya mtu ili kupata malipo kama hayo.

Mtu akituma ombi la FAP na kabla ya Nationwide Children's kubaini iwapo mtu huyo anatimiza masharti ya FAP, mtu huyo atume ombi la kustahiki kupata bima ya Medicaid, Nationwide Children's itaahirisha shughuli ya kubaini iwapo mtu anatimiza masharti ya FAP na haitahusisha Hatua zozote Zisizo za Kawaida za Ukusanyaji wa Madeni dhidi ya mtu huyo, hadi baada ya ombi la mtu huyo la Medicaid kukamilishwa na kutumwa na ubainishaji wa hali kutimiza masharti ya Medicaid ya mtu huyo kufanywa.

Orodha ya Watoa Huduma Wanaotoa Huduma za Dharura na Huduma Nyingine za Matibabu Zinazohitajika katika Nationwide Children's

Orodha inayoelezea kwa kina watoa huduma wanaotoa huduma za dharura na Huduma nyingine za Matibabu Zinazohitajika katika Nationwide Children's na iwapo huduma zao za kitaalamu zinalipiwa na mpango wa FAP wa Nationwide Children's inaweza kupatikana katika <http://www.nationwidechildrens.org/financial-assistance> au nakala ya karatasi inaweza kupatikana kwa kuwasiliana na idara zilizoordheshwa hapa chini, chini ya Anwani ya Mawasiliano.

Upatikanaji wa Sera ya Msaada wa Kifedha, Muhtasari wa Lugha Rahisi wa Sera ya Msaada wa Kifedha na Ombi la Msaada wa Kifedha

Ufikiaji wa Tovuti

<https://www.nationwidechildrens.org/your-visit/billing-and-insurance/financial-assistance>

Nakala za Karatasi

- Zinapatikana bila malipo kwa wagonjwa na mtu anayehusika baada ya kutuma ombi.
- Nakala za karatasi hupeanwa wakati wa kujiandikisha katika maeneo yoyote ya kujiandikisha au kujisajili katika chuo kikuu cha Nationwide Children's (ikiwa ni pamoja na Chumba cha Huduma ya Dharura) na maeneo yaliyo nje ya chuo.
- Barua na Maombi ya Msaada wa Kifedha hutumwa kwa wagonjwa na/au wazazi baada ya kutuma ombi.
- Taarifa zote za malipo zina fomu ya Ombi la Msaada wa Kifedha katika ukurasa wa mwisho wa taarifa pamoja na anwani ya mawasiliano ya idara ambayo inaweza kutoa usaidizi wa kutuma ombi.

Arifa na Maelezo Yanayotolewa kwa Wagonjwa Waliolazwa Hospitalini

- Ishara inayopatikana kwenye eneo lolote la kujiandikisha au kujisajili katika chuo kikuu cha Nationwide Children's (ikiwa ni pamoja na Chumba cha Huduma ya Dharura) na maeneo yaliyo nje ya chuo ya kuwashauri wagonjwa au watu wanaohusika kuhusu upatikanaji wa msaada wa kifedha.
- Simu zinazopigwa kiotomatiki zinazotoa msaada wa kifedha ambazo hupigwa baada ya kutolewa kwa taarifa ya pili ya malipo.
- Washauri wa Kifedha wa Nationwide Children's huwatembelea wagonjwa wanaohitaji msaada wa kifedha kwenye vyumba vyao au kwenye kliniki.

Kuarifu na Kuifahamisha Jamii Pana

- FAP, Muhtasari wa Lugha Rahisi wa FAP na Ombi la Msaada wa Kifedha vinaweza kupatikana vyote katika www.NationwideChildrens.org.
- Nationwide Children's hushiriki pia mara moja Muhtasari wa Lugha Rahisi wa FAP na Ombi la Msaada wa Kifedha na Vituo vya Afya Vilivyoidhinishwa Nchini katika Kaunti ya Franklin na pia kwa madaktari wa jamii ambao ni wanachama wa wafanyakazi wa Nationwide Children's ili hati zipatikane kwa urahisi kwa wagonjwa wanaotafuta huduma kwa huduma hawa.

Hati Zilizotafsiriwa

- Sera ya Msaada wa Kifedha, Ombi la Msaada wa Kifedha na Muhtasari wa Lugha Rahisi wa FAP vitapatikana kwa lugha inayozungumzwa na kila kikundi cha lugha ambacho hakielewi Kiingereza vizuri (LEP) ambacho kina idadi ndogo ya watu 1,000 au asilimia 5 ya wanaoishi katika Kaunti ya Franklin au kaunti nyingine ambazo zinaweza kuhudumiwa na Nationwide Children's. Mkurugenzi wa Akaunti za Wagonjwa atawajibika katika kukagua mahitaji ya lugha kila mwaka na kufanya matoleo yaliyotafsiriwa ya hati yapatikane jinsi inavyohitajika.

Anwani ya Mawasiliano

Washauri	Eneo	Simu
Nationwide Children's Washauri wa Kifedha	Ofisi ya Kujiandikisha 700 Children's Drive au kwa kuweka miadi katika maeneo yoyote ya Nationwide Children's	(614) 722-2070
Nationwide Children's Huduma kwa Wateja wa	Patient Accounts Huduma ya Simu Pekee	(614) 722-2055

**Imeidhinishwa na Kamati ya Fedha na Ukaguzi wa Mahesabu
ya Bodi ya Wakurugenzi wa Nationwide Children's Hospital
mnamo Novemba ____, 2020:**

Luke Brown
Afisa Mkuu wa Fedha

Tarehe